

## Nyenzo Nyinginezo

Kutumia kipengele cha kutafuta kwenye Chaguo za Utunzaji wa Watoto ni hatua moja tu katika mchakato wa kutafuta huduma kwa watoto; kuna nyenzo nyingine nyingi za kukusaidia kutafuta na kufanya uamuzi. Unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu:

- Ukadiriaji wa Hatua wa *Quality for ME* (*Ubora kwa ME),* ambao ni mfumo wa ukadiriaji na uboreshaji wa viwango vya ubora vya jimbo la Maine;
- Orodha za kuthibitisha za kutumia unapotembelea mipango;
- Maelezo kwa familia kuhusu ustawi wa watoto na utunzaji wa watoto wenye mahitaji maalum.

*Chapisho hili limefadhiliwa kupitia Nambari ya Ufadhili ya 90TP0028 kutoka Ofisi ya Utunzaji wa Watoto, Mamlaka ya Watoto na Familia, Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Marekani. Maudhui yake ni maoni ya mwandishi wake tu wala hayawakilishi maoni rasmi ya Ofisi ya Utunzaji wa Watoto, Mamlaka ya Watoto na Familia, Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Marekani.*

MAINE ROADS TO QUALITY
PROFESSIONAL DEVELOPMENT NETWORK
PO Box 9300
Portland, ME 04104-9300

Huduma kwa Watoto na Familia
Ofisi ya Idara ya Afya na Huduma ya Binadamu

MRTO PDN inafadhiliwa na Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Maine, Ruzuku ya Ustawi wa Utunzaji wa Watoto ya Ofisi ya Huduma za Watoto na Familia

UNIVERSITY OF SOUTHERN MAINE

Child Care Choices

childcarechoices.me

# Nyenzo yako ya Kutafuta Huduma ya Utunzaji wa Watoto katika jimbo la Maine

Swahili (1/21)



## Chaguo za Utunzaji wa Watoto ni Nini?

Chaguo za Utuzaji wa Watoto ni nyenzo ya mtandaoni ya jimbo la Maine ya kusaidia familia kutafuta na kupata maelezo kuhusu chaguo za utunzaji wa watoto.

Unaweza kutumia kipengele cha kutafuta ili utafute huduma ya utunzanji wa watoto itakayofaa mahitaji ya familia yako. Unaweza kupata maelezo kwenye tovuti yetu kuhusu:

- Aina za huduma za utunzaji wa watoto katika jimbo la Maine na nyenzo za kukusaidia kuchagua mpango unaoifaa familia yako
- *Quality for ME* (*Ubora kwa ME),* ambao ni mfumo wa ukadiriaji na uboreshaji wa viwango vya ubora vya jimbo la Maine;
- Maelezo kuhusu Uidhinishaji wa huduma za utunzaji wa watoto
- Nyenzo za familia, pamoja na usaidizi wa kulipia huduma ya utunzaji wa watoto

## Aina ya Utunzaji

Hizi ndizo aina za mipango ambayo imejumuishwa katika kipengele cha utafutaji kwenye Chaguo za Huduma kwa Mtoto:

**Utunzaji wa Watoto Unaotolewa kwa Familia:** Mipango hii hufanyiwa ndani ya nyumba za watu binafsi na mara nyingi huwafaidi watu wa umri mbalimbali.

**Kituo cha Kutunza Watoto:** Mipango hii huendeshwa katika kituo kilichojengwa hususan kuufaa utunzaji wa watoto. Mara nyingi katika vituo vya utunzaji wa watoto, watoto hao huwekwa katika makundi kulingana na umri.

**Shule ya Chekechea:** Mipango hii hutoa huduma kwa watoto kwa saa zisizodi 3 kwa siku. Baadhi ya shule za chekechea huandaa kipindi cha asubuhi na alasiri, lakini watoto wanaweza kuhudhuria kipindi kimoja tu kwa siku.

**Head Start (Mpango wa Maandalizi):** Huu ni mpango wa kitaifa ambao huwaandaa kimasomo watoto wa umri wa kutoka kuzaliwa hadi miaka mitano wanaotoka familia zenye kipato cha chini kwa kukuza uwezo wao wa kiakili, kijamii, na kihisia. Mpango wa Maandalizi huwahudumia wazazi na watoto wao wa umri wa kabla ya kujiunga na shule. Mipango mingi ya Maandalizi pia hutoa mipango ya Maandalizi ya Mapema, ambayo huwahudumia watoto wazawa, watoto wachanga, wanawake wajawazito na familia zao zenye kipato cha kiwango cha chini ya kiwango cha umaskini cha kitaifa. Mipango hii inaweza kuendeshwa nusu siku au siku nzima.

**Tufuate kwenye Facebook:**
**facebook.com/childcarechoicesmaine**

## Jinsi ya Kutafuta

Kipengele cha utafutaji kinakuwezesha kutafuta kulingana na:

- Aina ya utunzaji (utunzaji wa watoto unaotolewa kwa familia au kituo cha kutunza watoto);
- Anwani na umbali;
- Msimbo wa mji au eneo;
- Ukadiriaji wa hatua kwa *Quality for ME* (*Ubora kwa ME);*
- Umri wa watu wanaohudumiwa.

Matokeo hutolewa kwenye ramani na pia yakiwa katika orodha inayoweza kupakuliwa ambayo inajumuisha:

- Jina la mpango, anwani na nambari ya simu;
- Jina la mpango na umri unaohudumiwa na mpango huu;
- Ukadiriaji wa hatua kwa *Quality for ME* (*Ubora kwa ME);*
- Maelekezo ya kusafiri kwa gari;
- Maelezo ya leseni.

Ikiwa una maswali kuhusu utafutaji wako wa huduma ya utunzaji wa watoto, tafadhali piga simu 1-877-6805866 uwasiliane na Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Maine, Ofisi ya Huduma za Watoto na Familia.

## Wasiliana Nasi

Maine Roads to Quality Professional Development Network
childcarechoices@maine.edu
Tembelea tovuti yetu kwenye:
https://childcarechoices.me